**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWA VYOMBO VYA HABARI BAADA YA MAZUNGUMZO NA MHESHIMIWA DKT. FRANK-WALTER STEINMEIER, RAIS WA JAMHURI YA SHIRIKISHO LA UJERUMANI, 31 OKTOBA 2023**

***Mheshimiwa Rais Dkt. Frank-Walter Steinmeier;***

***Waheshimiwa Mawaziri;***

***Waheshimiwa Mabalozi;***

***Wageni Waalikwa;***

***Ndugu Waandishi wa Habari;***

***Mabibi na Mabwana:***

***Habari za mchana…!***

Leo, nchi yetu imepiga hatua nyingine ya kihistoria katika uhusiano wake na Ujerumani. Tumepata heshima ya kumkaribisha Mheshimiwa Dkt. Frank-Walter Steinmeier, Rais wa Jamhuri ya Shirikisho la Ujerumani hapa Ikulu, Dar es Salaam. Ninakushukuru Mheshimiwa Rais kwa kuitikia mwaliko wangu wa kutembelea Tanzania. Ziara yako ni ishara njema kuhusu umuhimu wa uhusiano kati ya nchi zetu mbili na inathibitisha dhamira yako Mheshimiwa Rais ya kuendeleza uhusiano huu wa kihistoria. Hivyo, ni heshima kubwa kwangu kukukaribisha

wewe na ujumbe wako hapa Ikulu ya Dar es Salaam. ***Karibu sana Tanzania!***

***Ndugu Waandishi wa Habari;***

***Mabibi na Mabwana:***

Leo asubuhi, mimi na Mheshimiwa Rais Steinmeier tumepata fursa ya kuzungumza kuhusu masuala mengi muhimu yahusuyo uhusiano na ushirikiano kati ya Tanzania na Ujerumani. Lakini hapa nitagusia baadhi ya masuala hayo.

**1.0 Ushirikiano wa kijamii na kiuchumi**

Sote tunatambua namna uhusiano wa nchi zetu mbili hizi umedumu kwa **miaka 60 sasa na unaendelea** kushamiri siku hadi siku katika nyanja mbalimbali hususan za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kupitia ujio wa Mheshimiwa Rais Steinmeier, nimefikisha shukrani zetu za dhati kwa watu na Serikali ya Ujerumani kwa namna inavyotuunga mkono kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo hapa nchini, hususan katika sekta za ***afya, maji, kilimo, elimu, utalii, utamaduni, michezo, ulinzi, maliasili, hifadhi ya mazingira,; na udhibiti wa fedha (yaani financial governance)***.

Katika mazungumzo yetu, tumesisitiza umuhimu wa kukuza ushirikiano huu kwa manufaa ya nchi zetu na watu wetu. Na katika hili, tumezielekeza timu za wataalam wa Tanzania na Ujerumani kuendelea na mazungumzo pamoja na mashauriano ya mara kwa mara yanayolenga kuboresha maeneo yaliyopo ya ushirikiano na kubainisha maeneo mapya yenye umuhimu kwa nchi zetu mbili. Katika hili, nimemhakikishia Mheshimiwa Rais, utayari wa Serikali ya Tanzania kuwa mwenyeji wa

mazungumzo yajayo ya ushirikiano wa maendeleo *(negotiations on development cooperation)* yatakayofanyika **mwakani (2024).**

## 2.0 Biashara na Mahusiano ya Uwekezaji kati ya Ujerumani na Tanzania

Katika mazungumzo yetu, tulisisitiza mchango muhimu wa biashara na uwekezaji katika kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuambatana na ujumbe wa wafanyabiashara muhimu kutoka Ujerumani. Leo, linafanyika kongamano la biashara ambapo Jumuiya ya wafanyabiashara kutoka Tanzania na Ujerumani zitakukutana, kujadiliana na kujenga mahusiano, lengo likiwa ni kufanikisha uwekezaji na kuongeza biashara.

Kongamano hili limetupatia fursa kwa Tanzania kuthibitisha azma yake ya kufanya biashara na Ujerumani na litabainisha fursa mbalimbali za biashara na uwekezaji zilizopo hapa nchini. Aidha, tumekaribisha wafanyabiashara na wawekezaji kutoka Ujerumani kuangalia fursa mbalimbali zinazopatikana katika sekta ya utalii, na katika uchumi wa bluu.

Ninapongeza kazi nzuri iliyofanywa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar na Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Kijerumani *(German Chambers of Commerce Abroad - AHK)* katika kuandaa kongamano hili ili kuwezesha biashara na kukuza uwekezaji kati ya Tanzania na Ujerumani.

## 3.0 Utalii

Tulizungumzia pia mchango mkubwa wa sekta ya Utalii katika uchumi wetu na kwamba, ili sekta hiyo iendelee kukua, ni lazima tuendelee kuimarisha ulinzi wa wanyamapori na utunzaji wa mazingira

na bioanui. Tunapongeza kazi nzuri iliyofanywa na Serikali ya Ujerumani, *Frankfurt Zoological Society* na mashirika mengine ya Ujerumani ambayo yamechangia sana katika kukabiliana na changamoto mbalimbali katika sekta hii ya utalii. Bado zinahitajika juhudi za makusudi, hasa kipindi hiki ambapo idadi ya watalii wanaotembelea Tanzania inazidi kuongezeka kutokana na uzuri wa vivutio vyetu.

**4.0 Mazungumzo kuhusu masuala yatokanayo na historia ya Ukoloni**

Kuhusu masuala yanayohusu historia yetu, ikiwemo masuala yatokanayo na historia ya ukoloni, nilisisitiza kuwa Tanzania iko tayari kuendelea na mazungumzo kuhusu historia hii na kuhusu wajibu wa Ujerumani kurejesha mali zilizochukuliwa enzi za ukoloni. Ninafahamu kwamba kuna juhudi za pamoja zinazoendelea kati ya taasisi zetu na taasisi zilizopo Ujerumani zinazolenga kufanikisha hili, ikiwemo kuwajengea uwezo wataalam na kuongeza uwezo wa makumbusho zetu.

Tunashukuru kwamba, Ujerumani inaendelea kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wetu na maafisa ili kuimarisha uwezo wetu katika maeneo haya yenye umuhimu tunapojiandaa kurejeshwa kwa vitu vilivyochukuliwa wakati wa ukoloni. Hatua ya kurejeshwa kwa mali hizo, ikiwemo mabaki ya binadamu, zana za mawe, na mabaki ya mimea na wanyama waliotoweka, itakuwa ni hatua muhimu katika kuhakikisha kuwa tunaweka historia sawa na kuitunza, na kufungua kurasa mpya katika historia ya mahusiano.

**5.0 Usawa wa Jinsia na Uwezeshaji wa Wanawake Kiuchumi**

Nchi zetu mbili zinaendelea kuweka msisitizo katika ajenda ya Usawa wa Jinsia na Uwezeshaji wa Wanawake Kiuchumi katika kuhakikisha maendeleo jumuishi. Tanzania imepiga hatua kubwa na takwimu zinadhihirisha maendeleo hayo. Pamoja na hayo, bado kuna

mengi yanahitaji kufanywa. Tunaishukuru Serikali ya Ujerumani kwa kuwasaidia wanawake wajasiriamali kupitia miradi mbalimbali hapa nchini. Nilisisitiza umuhimu wa kuendeleza ushirikiano ili kuongeza uwekezaji katika huduma bora za umma na binafsi zinazozingatia mahitaji ya wanawake *(gender-responsive public and private quality care);* kuweka mazingira wezeshi ya kisheria na kisera ili kuhakikisha kazi zenye staha kwa wanawake; kuongeza uwezo wa wanawake kupata na kusimamia rasilimali za uzalishaji; na kutekeleza mipango ya maendeleo inayozingatia mahitaji ya wanawake ili kupunguza idadi ya wanawake na wasichana wanaoishi katika umaskini.

**6.0 Demokrasia, Haki za Binadamu, Utawala wa Sheria, na Utawala Bora**

Kuhusu suala la demokrasia nchini, sisi sote tu mashuhuda wa hatua zilizochukuliwa na zinazondelea kutekelezwa nchini. Nilipoingia madarakani, nilikuja na **falsafa ya 4R** ambayo inakuza maridhiano ya kisiasa, ustahimilivu, mageuzi na kujenga upya. Nimeazimia kudumisha mafanikio ya tawala zilizopita na kuipaisha nchi yetu zaidi katika nyanja za demokrasia, haki za binadamu, utawala wa sheria na utawala bora.

Serikali ya Tanzania inaishukuru Serikali ya Ujerumani kwa msaada unaotoa katika kutekeleza mageuzi ya kidemokrasia na utayari wake wa kuendelea kufanya hivyo.

**7.0 Ushirikiano wa pande nyingi**

Katika mkutano wetu, pia tulipata fursa ya kujadili masuala yenye umuhimu kikanda na kimataifa. Tumekubaliana kuendelea kufanya kazi pamoja katika kuunga mkono juhudi za kumaliza migogoro na kurejesha utulivu barani Afrika.

**8.0 Kampuni Changa za Ubunifu (Startups)**

Rais Steinmeier na mimi tutapata fursa ya kukutana na kampuni tano za vijana wa Kitanzania wenye Kampuni Changa za Ubunifu, maarufu kama *Startups*. Kampuni hizi za Tanzania zinaendelea kuvutia uwekezaji mkubwa kutoka ndani na nje ya nchi, ikiwemo kutoka Ujerumani. Ninawapongeza sana vijana hawa kwa ubunifu wao mkubwa. Kama Serikali, tunatengeneza Sera ya Kampuni Changa za Ubunifu (Startups) kwa kushirikiana na wadau husika ili kuwajengea mazingira wezeshi na rafiki zaidi kwa kazi zao.

**Waandishi wa habari,**

Nimalizie kwa kusema kuwa: Ziara hii inathibitisha dhamira ya Serikali zetu mbili ya kuimarisha na kukuza ushirikiano na urafiki wetu kwa lengo la kuwanufaisha watu wetu.

Kwa mara nyingine tena, nakushukuru Mheshimiwa Rais kwa heshima uliyoipatia nchi yetu kupitia ziara yako. Nina imani kwamba ujio wako utachangia katika kuimarisha Zaidi ushirikiano kati ya nchi zetu katika sekta za biashara na uchumi; ushirikiano unaozingatia misingi ya kuheshimiana na kuaminiana.

Sasa, ninayo heshima ya kukukaribisha Mheshimiwa Rais uzungumze na waandishi wa habari.